

## Coronavirus 2019 (COVID-19)

### Ilani Muhimu kwa Wazazi na Wafanyakazi

Wasimamizi kutoka Shule za Umma za Kaunti ya Jefferson (JCPS) wamekuwa wakiwasiliana mara kwa mara na Idara ya Afya na Uzima wa Umma ya Louisville Metro (LMDPHW) kuhusu Ugonjwa wa Coronavirus 2019 (COVID-19) ili kuhakikisha kuwa tunachukua hatua zote tahadhari za kuzuia kuenea kwa virusi hivyo.

Hakuna kesi zilizodhibitishwa katika Kaunti ya Jefferson.

Kwa habari zaidi za kisasa kutoka kwa Vituo vya Kudhiboti Ugonjwa COVID-19, tembelea tovuti hii:

<https://www.cdc.gov/coronavirus/2019-ncov/index.html>

#### Unachohitaji Kujua

COVID-19 ni aina ya virusi ambavyo husababisha magonjwa ya miinuko mbalimbali kutoka homa ya kawaida hadi ugonjwa hatari zaidi wa kupumua.

#### Je, unaenezwa vipi?

- Kukohoa na kupiga chafya
- Mawasiliano ya kibinafsi ya karibu sana, kama vile kugusa au kusalimiana kwa mikono
- Kuguza kifaa au eneo lililo na virusi vile halafu kuguza mdomo wako, pua, au macho kabla ya kunawa mikono

#### Je, dalili ni zipi?

- Joto
- Kikohozi
- Ugumu wa kupumua
- Kuugua vikali

#### Je, naweza fanya nini?

- Nawa mikono yako mara kwa mara.
- Saidia wanafunzi wachanga kunawa mikono ya vizuri.
- Kaa nyumbani unapohisi kuugua, na shauriana na mtaalamu wa matibabu.
- Funika pua lako na mdomo unapokohoa au kupiga chafya.
- Zuia mawasiliano ya karibu na mtu yeyote aliye na dalili za homo au mafua.
- Ikiwa umekuwa na mawasiliano ya karibu na mtu anayetoa daliliza COVID-19 ambaye amesafiri hivi karibuni, tafadhali wasiliana na mtaalamu wa matibabu ili kudhibiti ikiwa unahitaji kupimwa.

JCPS tayari ina Mpango wa Tukio na Virusi vya Ugonjwa (PVEP) ambayo inaeleza hatua kadhaa ambazo wilaya inachukua ili kuingia wanafunzi na wafanyakazi. Tunataka kukujuza kuhusu hatua zetu na kujibu maswali yoyote unaweza kuwa nayo. Baadhi ya hatua kutoka PVEP zimo katika faili iliyopambatanishwa.

Ni muhimu kujua kwamba wilaya itazidi kufanya kazi moja na sheria za mitaani, majimbo na nchi. Tunakuhimiza kujisajili kwa arifu muhimu kutoka kwa JCPS kupitia Mjumbe wa Shule. Unaweza kujiunga kwa kutuma herufi "Y" kwa 67587.

Ikiwa una maswali zaidi kuhusu COVID-19, unaweza kuwasiliana na Vituo vya Udhibiti wa Kuzuia Magonjwa (CDC) kwa 1-800-232-4636.